**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA MHESHIMIWA ZAINAB R. TELACK WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO CHA BODI YA BARABARA CHA MKOA KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA TAREHE 13 FEBRUARI, 2018.**

***Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga,***
***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
***Waheshimiwa Wabunge,***
***Mheshimiwa Mstahiki Meya,***
***Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,***
***Makatibu Tawala Wasaidizi wa Sehemu na Vitengo,***
***Meneja wa TARURA Mkoa,***
***Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,***
***Wahandisi wote mliohudhuria,***
***Wageni waalikwa,***
***Waandishi wa Habari,***
***Mabibi na Mabwana.***
***Habari za asubuhi!!!!!!***

**Ndugu Wajumbe,**

Awali ya yote napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sisi sote afya njema na kutuwezesha kukutana tena kujadili na kutathmini shughuli mbalimbali za miradi ya barabara iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa. Nina kila sababu ya kuwashukuru Wajumbe wote kwa mahudhurio yenu kwa lengo la kufanikisha shughuli kubwa iliyopo mbele yetu ikiwa ni pamoja na kupanga mikakati ya kufanikisha usimamizi madhubuti na imara wa miradi ya maendeleo ya miundombinu katika Mkoa wetu.

**Ndugu Wajumbe,**

Kikao hiki ni cha kisheria na kinaongozwa na Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Wajumbe wote wa kikao hiki wameteuliwa kwa mujibu wa sheria ili kuunda chombo hiki muhimu katika ustawi wa miundombinu ya barabara zetu.

Ni matumaini yangu kuwa kila mjumbe atashiriki ipasavyo katika mjadala wa agenda mbalimbali za kikao hiki kwa kutoa mchango chanya wenye lengo la kuzidi kuuendeleza Mkoa wetu katika sekta ya barabara.

**Ndugu Wajumbe,**
Suala la matengenezo ya barabara, kutunza barabara na kuzifanya zipitike kwa muda mrefu ni letu sote kuanzia katika hatua ya Kijiji hadi Taifa.

Kumekuwa na changamoto nyingi katika Sekta ya barabara katika Mkoa wetu zikiwemo wananchi kutokujali au kutoelimishwa vya kutosha juu ya utunzaji wa Barabara kwa kulima, kujenga, kufanya biashara ndogo ndogo na hata kuegesha magari kwenye hifadhi ya barabara, hii huchangia barabara hizo kuharibika mapema na wakati mwingine kuzifanya zisipitike kwa urahisi hasa sehemu za miji yetu na Makao Makuu ya Wilaya. Aidha, zipo changamoto zingine zinazoikumba miundombinu yetu, kama vile mitaro ya barabara kuziba na madaraja kujaa mchanga na kutopeleka au kutoa maji hivyo kutokufanya kazi iliyokusudiwa, niwaombe katika maeneo yenu kuweka utaratibu mzuri wa kuwaelimisha Wananchi.

Pia, ili kukabiliana na changamoto hizi Serikali yetu kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilianzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini inayojulikana kama TARURA.

TARURA imeanzishwa ili kuchukua majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Ni matumaini yangu kuwa Mratibu wa TARURA wa Mkoa leo katika kikao hiki atapata nafasi ya kutufafanulia muundo na Majukumu ya TARURA ili wajumbe wote waweze kuelewa na kusaidia utekelezaji mzuri wa majukumu yake.

**Ndugu Wajumbe,**
Barabara nyingi katika Mkoa wetu zinaharibika kwa sababu ya magari yaliyozidi uzito kupita katika Barabara zinatotakiwa kupita gari zenye uzito mdogo. Kwa mfano barabara ya kutoka Lubaga kuelekea Old shinyanga mpaka Bubiki na Barabara ya kutoka Kolandoto kuelekea Mhunze hadi Lalago zimekuwa zikiharibika mara kwa mara.
***Naagiza:*** *Wakala wa Barabara wa Mkoa kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama Barabarani kuhakikisha magari mazito hayapiti kwenye barabara zisizoruhusiwa.*

**Ndugu Wajumbe,**
Kutokana na Elimu duni inayotolewa kwa wananchi wetu bado tatizo la kupitisha mifugo barabarani husababisha uharibifu mkubwa kwenye miundombinu hiyo na kusababisha Serikali kurudia matengenezo mara kwa mara.

*Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa simamieni hili kwa kuhakikisha kwamba sheria ndogo za Halmashauri zinafuatwa. Mara kwa mara nimekuwa nikiwaagiza kuhusu suala hili lakini halitekelezwi ipasavyo.*

**Ndugu Wajumbe,**
Baadhi ya Wakandarasi wamekuwa sio waaminifu katika utekelezaji wa kazi za Barabara kwa kutofuata mikataba yao.
Kwa mfano, Manispaa ya Shinyanga iliingia mkataba na Mkandarasi "Termite Investment" wa Dar es Salaam wa kiasi cha sh.314,834,505.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za kata ya Kambarage, Ndala na Masekelo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa muda wa siku 120, lakini Mkandarasi huyo wakati wa utekelezaji wa kazi aliacha vifusi barabarani zaidi ya miezi miwili na kuleta usumbufu kwa wananchi, alipobanwa alisambaza vifusi hivyo na kusimamisha kazi bila taarifa. **Hivyo Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imelazimika kuvunja mkataba ili atafutwe** Mkandarasi mwingine.

Halmashauri ya Wilaya ya Msalala iliingia mkataba wa sh.397,734,600.00 na Umoja wa Makandarasi Tingwa Co.Limited na Derick Co. Limited kwa ajili ya matengenezo ya barabara, Wakandarasi hawa walifanya kazi yenye thamani ya sh.123,569,600.00 **lakini Halmashauri**

**ilishindwa kuwalipa sh.57,404,600.00, na kusababisha Wakandarasi hao kushindwa kumaliza kazi kwa muda uliopangwa jambo lililopelekea Halmashauri kuvunja mkataba.**

Pia tunayo matengezo ya Barabara ya Old Shinyanga inayojulikana kwa jina la Shinyanga – Bubiki (jina la mkataba), Barabara hii ina Wakandarasi wawili (2) ambao ni Salumu Motor Transport (SAMOTA) wa Nzega Tabora, yeye anajenga barabara yenye urefu wa mita mia saba (700) kwa kiwango cha Lami,kwa gharama ya sh.543,281,912.00 alianza tarehe 02/07/2017 na anatarajiwa kukabidhi tarehe 28/02/2018, mpaka hapo amefikia asilimia 85 ya kazi.

Mkandarasi wa pili ni Jonta Inestment Co. Ltd wa Shinyanga, yeye anatengeneza barabara yenye urefu wa mita mia tatu (300) kwa kiwango cha Lami kwa gharama ya sh.242,513,600.00 na anatarajia kukabidhi tarehe 28/02/2018 mpaka sasa amefikia asilimia 60 tu ya kazi.

*Nataka kuwaambia wasimamizi mnaosimamia matengenezo ya barabara, Hakikisheni mnasimamia kikamilifu matengenezo hayo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ujenzi wa Barabara, na katika hili ikibainika Mkandarasi amefanya kazi chini ya kiwango kinachotakiwa sitamruhusu aendelee kufanya kazi katika Mkoa wetu.*

**Ndugu wajumbe,**

**Mwisho lakini sio katika umuhimu**, napenda kumaliza kwa kuwaomba ninyi nyote kwa pamoja mshirikiane na Mkoa katika mpango kabambe wa kupanda miti ili kuufanya Mkoa wetu kuwa miongoni mwa Mikoa yenye kupata mvua za kutosha. Tumekwisha anza kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri zetu ikiwemo kwenye taasisi za shule, pembezoni mwa barabara, maeneo ya makazi n.k. kila kiongozi akiwaelimisha wananchi kuhusu hili naamini tutafanikisha azima ya Serikali.

***Baada ya maelezo hayo, sasa natamka kwamba kikao hiki cha Bodi ya Barabara nimekifungua rasmi.***

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!**